# *VISHAWISHI*

Hilo ni jambo jema. Nafikiri inatupasa kusimama tunaposoma Neno Lake. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kwa hiyo hebu na tusimame kidogo tu, tunaposoma Neno Lake. Ninasoma, usiku wa leo, kwa ajili ya somo la Maandiko linalopatikana katika Kitabu cha Isaya, mlango wa 6. Sikilizeni kwa makini.

> *Katika* siku zile *alipokufa mfalme Uzia nalimwona Bwana ameketi katika kiti cha enzi, kilicho juu sana . . . kuinuliwa sana, na pindo za vazi lake zikalijaza hekalu.*
>
> *Juu yake walisimama maserafi; kila mmoja alikuwa na mabawa sita; kwa mawili alifunika uso wake, na kwa mawili alifunika miguu yake; na kwa mawili aliruka.*
>
> *Wakaitana, kila mmoja* na mwenzake, *wakisema, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ni BWANA* Mungu *wa majeshi; dunia yote imejaa utukufu wake.*
>
> *Na misingi ya vizingiti ikatikisika kwa sababu ya sauti yake aliyelia, nayo nyumba ikajaa moshi.*
>
> *Ndipo niliposema, Ole wangu! kwa maana nimepotea; kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wenye midomo michafu; na macho yangu yamemwona Mfalme, BWANA wa majeshi.*
>
> *Kisha mmoja wa maserafi wale akaruka akanikaribia; naye alikuwa na kaa la moto mkononi mwake, ambalo alikuwa amelitwaa kwa makoleo toka juu ya madhabahu;*
>
> *Akanigusa kinywa changu kwa kaa hilo, akaniambia, Tazama, hili limekugusa midomo yako, . . . uovu wako umeondolewa, na dhambi yako imefunikwa.*
>
> *Kisha nikaisikia sauti ya Bwana, akisema, Nimtume nani, naye ni* nani *atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi hapa, nitume mimi.*

2 Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

3 Baba, "ole," tunajisikia vile vile Isaya alivyojisikia, "Ole wetu! Kwa maana macho yetu yamemwona Mfalme, Bwana wa Utukufu." Tunakushukuru, Bwana, ya kwamba kuna njia ya utakaso, usiku wa leo, ambayo inaweza kugusa si midomo yetu tu bali mioyo yetu na nafsi zetu, na kutusafisha na uchafu wetu wote. Kwa kuwa ndivyo ilivyo, hakika, tunaishi miongoni mwa watu wenye midomo michafu, na midomo yetu, pia, ni michafu. Tunaomba ya kwamba yule Roho Mtakatifu mkuu atakuja na kuigusa midomo yetu na mioyo yetu kwa upako, Moto wa Roho Mtakatifu toka kwenye madhabahu ya Mungu, na kutusafisha

na kutokuamini kwetu kote na mashaka, ili Yeye apate kuingia na kufanya makao Yake pamoja nasi. Kwa kuwa, tunampenda, na tunamsujudu, na tunamwabudu. Tunaomba, Baba, usiku wa leo, kama kuna mtu yeyote hapa ambaye hajapata ule mguso unaosafisha wa yule Roho Mtakatifu mkuu, huo Moto wa Mungu, na iwe kwamba usiku huu kuwa kazi hii itafanyika ndani yao kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Tunaomba hilo katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

4 Sasa mimi ni-. . . tutajaribu kutoka mapema. Sitaki ninyi mkose shule ya Jumapili. Sasa, haidhuru kwenu ninyi kukosa kazi ya siku moja, hamtaikosa hiyo sana; bali nitawaweka mpaka saa tatu na nusu, ama kitu fulani, kama kwenye usiku ule mwingine. Bali msikose shule ya Jumapili, hata mkifanyaje.

Sasa somo langu usiku wa leo ni: *Vishawishi.*

5 Tunataka kusoma hadithi hii, inabidi tufungue Mambo ya Nyakati wa Pili, mlango wa 26, na mngeweza kuusoma. Huyu Uzia alikuwa ni mvulana mchungaji. Naye, Mambo ya Nyakati wa Pili 26 inatwambia, alitiwa mafuta kuwa mfalme kwenye umri wa miaka kumi na sita. Na baba yake Uzia, mtu mcha Mungu. Na mtu huyu alikuwa ni mtu mwadilifu, akiwa na wazazi wacha Mungu, "Alifanya yaliyo maadilifu machoni pa Bwana." Sasa tunaona ya kwamba kwa kawaida . . .

6 Na—nafikiri leo, shida yetu kubwa, kuhusu yale tunayoamini kwamba ni uhalifu wa watoto, ni uhalifu wa wazazi, uhalifu wa nyumbani. Watu we—wetu waliyaacha mambo ambayo wao—wao walipaswa kudumu nayo. Kanisa likawa vuguvugu ama baridi, na wa—watoto wakatoka na kuingia ulimwenguni.

7 Sasa Hollywood inatoa filamu nyingi sana na—na televisheni, na kadhalika, ambazo hata hazijakaguliwa, ambamo watu hulaani na—na—na kutumia Jina la Mungu bure. Na—na ilikuwa ni kawaida kwamba ni vibaya kwa watoto katika makanisa ya utakatifu kwenda kwenye—kwenye—kwenye sinema ama maonyesho ya picha, na sasa Shetani ameruka hatua moja mbele, kwa kuleta hayo moja kwa moja nyumbani, katika namna ya televisheni, na tena hazijakaguliwa, na—na kadhalika. Na hiyo ndiyo njia ya Shetani ya kuingia polepole.

8 Kama vile sileji ya kale ilivyokuwa. Wengi wenu hamwikumbuki, maana ninyi mna umri mdogo sana. Kulikuwa na burudani ya watoto; uliketi kwenye sileji yako na kuzunguka-zunguka tu, huku na huko. Kulikuwa na shimo, poromoko, na kila mtu angemsai mwingine, kwamba ni nani angeweza kusogea karibu sana nalo. Basi punde si punde, kabla hujawa na habari, [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.] wewe huyoo chini ulianguka.

9 Hivyo ndivyo dhambi ilivyo. Usichezecheze nayo. Usiangalie jinsi unavyoweza kuikaribia. Angalia jinsi unavyoweza kukaa

mbali nayo. Unaona? Usijasirie chochote. Kama utajasiria. . . Mimi sitaki kujasiria.

10 Mzee mmoja Msikoti, wakati mmoja, watu walisema, alikuwa akienda kuvuka mlima. Na magari ya farasi yalikuwa yakingojea, kila mmoja alitaka kumvusha. Akasema, "Ninataka kuvushwa na saisi aliye bora kabisa."

11 Mmoja wao akasema, "Vema, ninaweza kuendesha kundi la farasi wangu sita kwa mwendo wa mbio sana kukaribia—kukaribia inchi kumi ya ukingo unaouzunguka mlima ule." Kuanguka, ni mauti. Kasema, "Mimi ni saisi mzuri kutosha kuendesha farasi wangu, kwa usalama, kuuzunguka huo pale, kukaribia inchi kumi toka kwenye magurudumu yangu, na nisianguke."

12 Yule mwingine akasema, "Mimi ninaweza kuzidi hapo. Ninaweza kuendesha kukaribia inchi sita, ama inchi nne, na katu nisianguke."

Akasema, "Na wewe je, bwana?"

13 Kasema, "Vema, sijui. Sipendi kufanya hivyo. Mimi—mimi hung'ang'ania tu ukingoni."

Akasema, "Wewe nipeleke." Hilo ni sawa. Huyo ndiye.

14 Si kadiri unavyoweza kuja karibu, na jinsi unavyofikiria umekingwa vizuri, kaa tu mbali na dhambi kadiri uwezavyo kukaa. Wewe kaa mbali tu uwezavyo. Unasema, "Vema, ninaweza kufanya jambo *hili*. Hakuna madhara katika kufanya *hili*." Vema, kama kuna swali niani mwako, usifanye jambo hilo kamwe. Po pote palipo na swali, usipakaribie. Halafu, unaona, ndipo unaishi hakika kabisa kwa imani, kama hakuna swali. Kukiwa na swali, basi liache, usilikaribie kabisa.

15 Nami ninafikiri ya kwamba mara nyingi kwamba wazazi ndio wanaokengeuka. Ninajua ya kwamba kuna wakati mwingine ambapo shu—shule, na kadhalika. Na shule ya Jumapili kama nusu saa, ama saa moja Jumapili asubuhi, nao ulimwengu unakuwa na hao watoto kwa wakati wote wa juma uliosalia, na unawashindilia kuliko mwalimu. Na mara nyingi, mara nyingi mno, mwalimu ana kitu kidogo anachofundisha kila mwezi wa tatu, huku akijipaka rangi midomo yake na kutengeneza nywele zake, akiwaacha watoto wajishughulikie vizuri wawezavyo.

16 Na halafu huko nyumbani hawapati mafunzo yoyote ya Kikristo hata kidogo. Mama yuko mitaani mahali fulani kwenye karamu ya kadi, na baba yuko huko kichochoroni kwenye mchezo wa kuviringisha tufe, na—na dada yuko huko nje na mtu fulani mwenye gari la anasa. Nawe huyo hapo, unaona. Nini, tunaenda—tunaenda wapi? Unaninii tu, ni ninii tu. . . Inatisha. Na halafu tunaona ya kwamba mambo haya yote yanaenda pamoja. Kadogoo yuko huko nje, akizurura mtaani, akiendesha

pikipiki yake. Na, loo, na baadhi yao kule wakicheza gofu, na wengine wakicheza kamari, na ni kitu kimoja ama kingine cha kujifurahisha tu. Na kanisa linayaachilia.

17 Mara nyingi, basi wana halmashauri pale; kama ikitokea kwamba mchungaji aguse waya fulani mdogo pale ambao ulikuwa—ulikuwa kwa namna fulani ni kinyume kidogo, ama aseme jambo fulani juu ya jambo hilo, halmashauri hiyo ingemchukua, jina lake lingepelekwa makao makuu na angetengwa na ushirika. Kwa hiyo, unaona, imekuwa ni jambo la posho, badala ya mtumishi aliyetiwa mafuta kuihubiri Injili. Unaona? Hiyo ni kweli. Linakuwa ni jambo wanalotaka. Ni—ni suala la posho. Inawabidi wakae humo, wapate mshahara mzuri. Sikiliza, ndugu, Mungu na amrehemu mtu ambaye angeuza haki zake za mzaliwa wa kwanza kwa jambo hilo. Sikilizeni!

18 Tunahitaji mtu atakayeshika Injili, mikono mitupu, si kwa glavu ya aina yoyote ya kimadhehebu. Kuliweka tu pale jinsi lilivyoandikwa, na kuacha vibanzi viruke popote vinapotaka. "Kama kiatu kikikutoshea," mama alizoea kusema, "kivae." Kasema, "Usipogoe sugu yako." Sasa, kwa hiyo tuna mambo hayo ambayo tunapaswa kuwa tukiyasikiliza.

19 Sasa, huyu mfalme, Uzia, akiwa mtoto mzuri sana hivyo. Alikuwa na baba mcha Mungu. Mama yake alitokea Yerusalemu, na baba mcha Mungu aliyemtangulia kuwa mfalme, na mafundisho ya namna hiyo yakamwingia sana mvulana huyo.

20 Mimi si Mwanademokrasia wala Mripablikani. Nilipiga kura moja tu, na hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya Kristo. Na Yeye ni ninii—Yeye ni . . . nitashinda kwa Hiyo.

21 Sasa, na—nafikiri Rais aliye mkuu kuliko wote, hata hivyo, tuliyepata kuwa naye, alikuwa ni Abraham Lincoln. Si kwa sababu yeye alikuwa ni Mkentake, pia, bali ilikuwa ni kwa sababu mtu huyo asili yake ilikuwa ni duni. Na vitabu vyote mtu huyo alivyopata kuwa navyo, tangu wakati alipokuwa mvulana mdogo, mpaka alipokuwa mtu mzima, karibu na utu uzima, vilikuwa ni Biblia na—na kitabu cha Bunyan kiitwacho *Safari ya Msafiri*. Unaona, hivyo viliumba tabia yake (kitu gani?) akawa yule "Abe mwaminifu." Yeye . . . Unachosoma, unachofanya, huumba tabia yako. Ki—kinaonyesha vile ulivyo. Na sasa, unaona, yeye alisoma mahali ambapo "kama ulifanya kosa, ulililipia; kama ulifanya haki, Mungu angeliiunga mkono," na hilo lilimfanya kile alichokuwa. Na mama yake, mwanamke m—mcha Mungu, pia. Yeye alisema, "Kama kuna sifa zozote za kupewa mtu yeyote, ilikuwa ni mama mcha Mungu," aliyemlea vizuri. Sasa huyo alimfinyanga kuwa Rais, nafikiri, ningesema angalau mmoja, kama si aliye mkuu kuliko wote, tuliokuwa nao. Aliibuka kutoka mahali duni kabisa, ndipo Mungu akamfanya Rais kwa kuwa alikuwa ni mtu mwaminifu na mtu mwadilifu.

22 Sasa, tunaona ya kwamba mvulana huyu alikuwa naye yuko vile vile. Akiwa na hawa wazazi wacha Mungu, alifanya yale yaliyokuwa mema. Alipofanywa mfalme, na wakati alipokuwa na umri wa miaka kumi na sita, alipuuza siasa zote na maoni ya watu wa siku zake, na akamtumikia Mungu kwa uchaji. Hilo lilimfanya kuwa mfalme halisi. Kupuuza siasa na maoni ya watu wa kisasa, na kumtumikia Mungu kwa uchaji, hilo lilikuwa ni jambo zuri sana. Ufalme wake, Mungu aliubariki, ulikuwa ni mkuu sana mpaka ukawa ni wa pili toka kwa ule wa Sulemani. Na Sulemani alikuwa na ule mkuu sana uliowahi kuwako; lakini mvulana huyu alikuwa ni wa pili toka kwa Sulemani, katika ufalme wake.

23 Ulikuwa ni m—msaada mkubwa kwa yule nabii kijana Isaya, naye akiwa ni kijana wakati huo, akikua tu. Kwa kuwa alizaliwa akiwa nabii, aliangalia ushawishi ambao mtu huyu alikuwa nao juu ya watu; na akaona mahali ushawishi wake ulikotoka, kwa maana yeye alimtumaini Mungu, kwa dhati. Naye alikuwa. . . Aliona tena, Isaya aliona, jinsi ambavyo Mungu atawabariki wale watakaokuwa waaminifu kwa Neno la Mungu.

24 Sasa tunatambua ya kwamba jamaa huyu kijana alitaka kudumu na kanuni za mambo ambayo Mungu alisema. Alitii amri Zake. Uzia asingegeuka kulia wala kushoto. Yeye alidumu moja kwa moja na yale Neno liliyosema, ndipo Mungu akamheshimu na kumbariki katika kila alichofanya, akamneemesha, akaendelea kwa uaminifu. Ni m—mfano wa jinsi gani huo kwa kijana yeyote!

25 Nafikiri kama tungalikuwa na watu leo, makanisa yetu wanaodai kwamba wao ni Wakristo, kama wangaliyaacha mambo ya ulimwengu na waishi maisha ya namna hiyo, ingewashawishi Wakristo wachanga kufanya hivyo. Lakini, leo, wakati wanapoachilia mambo, na kunywa pombe na kuvuta sigara, na kufanya yasiyofaa, na bado wangali wanajaribu kushikilia ushuhuda wao kama Ukristo, hilo linaweka jiwe baya la kujikwaa katika njia ya watu wengine, na inafanya mambo kuwa magumu sana.

26 Kumbukeni, Biblia ilisema, "Ninyi ni nyaraka zilizo hai, zilizoandikwa, zinazosomwa na watu wote." Sasa, watu wengi hawatasoma Biblia, bali Mungu amekufanya wewe mwakilishi aliye hai. Wewe ni barua inayotembea, unapaswa kuwa Biblia inayotembea, Kristo ndani yako. Unapaswa kuwa Neno la Mungu linalotembea. Na kama ukikiri kuwa Mkristo, nawe sivyo ulivyo, ushawishi wako, ninii yako. . .Kile unachoshawishi, kitakufanya uwajibike kwa nafsi za wengi ambao umewakengeusha, mbali na Kristo, katika Siku hiyo ya Hukumu.

27 Nafikiri inatupasa, usiku wa leo, kuwazia jambo hilo, kwa kuwa kila mwanamume, mwanamke, mvulana na msichana,

anajua kwamba unakuja Hukumuni. Huenda ukaepuka *hili*, *lile*, ama *linginelo*. Huenda ukaepa kodi ya mapato, na huenda ukaepa Mapato ya Ndani ya nchi. Huenda ukafanya jambo moja ama lingine. Huenda uliendesha gari kupita mwendo ulioruhusiwa na polisi wasikushike. Lakini, siku moja, Hukumu itakushika. Hiyo ni hakika!

28 "Nasi tunajua ya kwamba mwanadamu hana budi kufa, na baada ya hilo ni Hukumu." Kifo si jambo gumu. Suala ni hiyo Hukumu baada ya kufa, hiyo ndiyo sehemu mbaya. Na huko, yale umefanya maishani, na jinsi ambavyo umewashawishi wengine, itakubidi kujibu kwa jambo hilo kwenye Siku ile.

29 "Ni zaidi sana vipi inavyotupasa kuweka kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo upesi, ili tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu, tukimtazama," si kanuni ya imani, madhehebu, mtu fulani mwingine, bali, "Yesu Kristo mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza Imani yetu."

30 Jinsi tunavyopaswa kuyawazia mambo hayo, enyi marafiki, kwa makini mno na kwa uchaji, tunapoona Siku hii ikikaribia, na tukijua ya kwamba wakati wowote kurasa zako za maisha, kile kitabu, kinaweza kufungwa usiku wa leo, na kesho itakuwa umechelewa sana kufanya jambo hilo. Usiahirishe yale unayoweza kufanya leo, kwa ajili ya kesho, kwa maana huenda kesho isije kamwe. Wanaume na wanawake, wavulana kwa wasichana, huenda wameketi hapa usiku wa leo, watakuwa kwenye chumba cha maiti kabla ya mapambazuko. Ni kweli. Na ndipo kitabu chako kimefungwa, nawe hutapata nafasi nyingine kamwe. Huenda hii ikawa ndiyo nafasi ya mwisho utakayopata kuwa nayo. Wazia jambo hilo, kwa makini. Unasema, "Vema, labda siyo." Labda siyo, bali ingeweza kuwa. Lakini, kumbuka, siku moja kitabu hicho kitafungwa, pamoja na yale unayofanya sasa.

31 Na hasa sana ninyi watu mnaodai kuwa ni Wakristo, jitengeni na mambo ya ulimwengu. Achaneni na ulimwengu. Jitengeni nao, kwa kuwa mtu fulani anakuangalia. Mtu fulani anakuangalia. Nawe si kwamba tu utajipeleka kule, bali utawapeleka wao mahali pabaya, nawe itakubidi kuwajibika kwa ajili ya ushawishi wako.

32 Jinsi ambavyo nabii huyu alivyomwangalia mtu huyu, na kuona ya kwamba Mungu alimbariki, na jinsi ulivyokuwa ni ushawishi wa ajabu jinsi gani! Jinsi ambavyo mtu huyo alivyofanikiwa, yale Mungu aliyomfanyia. Aliishi ma—maisha ambayo yalikuwa ni mazuri sana, yaliyobarikiwa na Mungu, wala asingegeuka upande wa kulia wala wa kushoto.

33 Sasa hapa tunaona mfano mwingine hapa katika mtu huyu, mtu huyu Uzia, mfalme mkuu ambaye wakati mmoja alitembea pamoja na Mungu. Biblia ilisema, "Wakati mfalme huyu

alipojisikia ya kwamba yuko salama, alipojisikia ya kwamba alikuwa yuko sawa, ndipo alipojitukuza moyoni mwake, kwa majivuno."

34 Hebu nisimame hapa kwa kusema jambo hili, kwa uchaji, ndugu yangu, dada. Mungu amewafanya ninyi kuwa wasikilizaji wangu usiku wa leo. Sina budi kuwa mwaminifu kabisa katika yale ninayosema, nanyi inawapasa kusikiliza kwa makini sana.

35 Hiyo ndiyo shida waliyo nayo watu wengi siku hizi. Wanafikiri . . . Tuna baadhi ya ndugu zetu wahudumu, wengine wao wanafikia mahali, labda, na wanazo huduma kuu, mpaka wanajisikia wako salama. Tumekuwa na jambo hili, tunajua kwamba jambo hili ni kweli. Wahudumu wengi nchini leo wameanza kunywa pombe. Baadhi yao wanafikiri, "Vema, nimejenga ufalme wangu mdogo pande zote. Hakuna sababu kwangu . . . Hao watu wananipenda sana, mpaka hawatajali hata kidogo kama nikifanya jambo *hili* ama nikifanya *lile*." Hebu nikwambie, ndugu, yupo Mmoja Ambaye anaangalia, na huyo ni Mungu. Hakuna mtu aliye salama nje ya Mungu.

36 Mara nyingine basi tunafikia mahali, tunawazia, "Mungu anatubariki. Amenipa Kadilaki. Amenipa kazi bora zaidi. Amenipa *hili*." Hiyo siyo ishara ya kwamba huwezi kuzigeuzia mbali baraka Zake.

37 Unaposhikwa na majivuno, na kujisikia, "Vema, wakati mmoja nililala usiku kucha na kuomba, wakati mmoja nilifanya jambo *hili* na ninafanya jambo *lile*, bali sikulifanya tena," uko mahali pa hatari.

38 Hiyo ndiyo shida iliyopo kwa watu wetu Wapentekoste. Wakati, huko nyuma, muda mrefu uliopita, tulipokuwa na misheni ndogo huko chini mahali fulani pembeni, na wanawake wasio na soksi ndefu na wakipiga tari kule chini, ilibidi waombe usiku kucha, na kila kitu; polisi waliwaweka ndani, nanyi mkakaa gerezani, na kadhalika. Mliomba. Makanisa, madhehebu yote, waliwacheka na kuwadhihaki. Bali sasa Mungu amewainua, mpaka mna baadhi ya makanisa mazuri sana nchini, madhehebu makubwa yenye nguvu, nanyi mmeanza kujisikia mko salama. Iweni waangalifu, hapo ndipo mnapoingiwa na majivuno. Halafu, wakati Mungu anapotuma kitu Fulani, hamwezi kukipokea, tena, kwa sababu tayari mmeshuhudia kitu *hiki*. Ndipo mnaanza kujisikia mko salama, huo ndio wakati ambapo mko njiani kuelekea kwenye kuanguka kwenu. Hilo linahusu madhehebu. Hilo linahusu mataifa.

39 Angalieni taifa letu, wakati mmoja lilikuwa ni moja ya mataifa maadilifu sana ya ulimwengu. Liangalie leo, ni taifa la kuchekwa ulimwenguni, chafu kuliko kitu chochote nikijuacho.

40 Niliposhuka kwenye ndege, na nikaingia huko Roma, na nikaenda hadi Saint Angelo, kuingia kwenye yale mapango ya kuzikia, nilitahayarika nilipoona kionyo kwenye ninii—mapango

ya kuzikia ya Saint Angelo, kilichosema, "Onyo kwa wanawake wote Wamarekani! Tafadhalini vaeni nguo kabla ya kuingia kwenye mapango haya, ili kuwaheshimu wafu." Wakiingia ndani mle wamevaa kaptura, na suruali ndefu, katika mahali kama Roma; na tena basi ilibidi kuwaambia, wanawake Wamarekani, "kuheshimu wafu; na kuvaa nguo." Mbona, imekuwa ni uvundo kwenye mapua! Na hela zetu zote za ng'ambo, na mikopo tuliyotoa, na kila kitu cha jinsi hiyo, kamwe havitanunua urafiki.

41 Kitu tunachohitaji katika taifa hili, na wala kabisa hatutakipata, bali tunachohitaji ni wa—wakati wa kuisafisha nyumba; si kusafisha nyumba kisiasa, bali ni ufufuo uliotumwa na Roho Mtakatifu ambao utalisafisha kutoka kichwani hadi miguuni. Hicho ndicho makanisa yetu yanachohitaji. Hicho ndicho watu wetu wanachohitaji. Hicho ndicho, sisi kama watu binafsi, tunachohitaji. Huo ndio ushawishi wetu... Tunapojivuna na kusema, "Mimi ni Mpentekoste. Nilinena kwa lugha. Nilipiga makelele. Nilicheza katika Roho." Huenda ulifanya jambo hilo, bali hebu nikwambie jambo fulani, ndugu, hilo si usalama kwako, hata kidogo.

42 Tunaona ya kwamba wakati Uzia alipotukuka moyoni mwake, tunaona ya kwamba Mungu alimpiga. Yeye alifanya nini? Alijaribu sana kujaribu kupachukua mahali pa mhudumu. Alifikiri kwa sababu ametukuka, Mungu alikuwa amembariki, akamfanya mtu mkuu, angeweza kufanya tu lolote alilotaka.

43 Nilimsikia kijana mwanamume mmoja akiniambia si muda mrefu uliopita, alisema, "Unajua, Mungu ananipenda sana, Ndugu Branham, Yeye huniacha nifanye tu lolote ninalotaka. Hajali."

44 Ninasikia mengi sana siku hizi juu ya Mungu kuwa ni Mungu mzuri. Ni Mungu mzuri. Sikanushi hilo. Yeye ni Mungu mzuri. Lakini pia Yeye ni Mungu wa hasira. Utakatifu Wake unataka kuwapo kwa haki. Sheria yake inahitaji hukumu. Kusipokuwa na hukumu kwa sheria, sheria haina nguvu. Itafaa nini kusema, "Ni kukiuka sheria kupita kwenye taa hizi nyekundu hapa chini," bila ya kuwa na adhabu nyuma ya sheria hiyo? Unaona, isingekuwa ni sheria. Wasingeweza kufanya jambo lolote juu ya jambo hilo; hakuna adhabu. Kuna adhabu ya kukiuka amri za Mungu, na, itaninii, itakubidi kulipa hadi senti ya mwisho kabla hujaachiliwa.

45 Sasa watu wengi siku hizi hufanya kosa hilo la kuhuzunisha kama jamaa huyu alivyofanya, wakati alipojiinua, akajitukuza, akafikia mahali ambapo alikuwa ameshika kila kitu mikononi mwake, alijisikia salama, "Mungu ananipenda sana, mpaka hakuna kitu kinachoweza kunisumbua sasa." Wakati alipofanya jambo hilo, alijitupa kwenye hali ile ile ambayo Nebukadreza alijitupa wakati mmoja, kama vile ninyi wasomaji wa Biblia

mnavyojua. Ndipo tunaona ya kwamba alipigwa kwa ukoma kwa sababu alijaribu kupachukua mahali pa mhudumu.

46 Si muda mrefu uliopita, ninazungumza kimataifa kwa ajili ya Wafanyabiashara wa Full Gospel. Hivi majuzi, nilikuwa nimeketi mahali fulani, ilikuwa ni kule Jamaica, tulikuwa na mkutano.

47 Ninawapenda, kwa sababu ni watu kutoka katika makanisa yote. Inanipa nafasi ya ku—kuhubiri. Mara nyingine makanisa hayataunga mkono, bali wafanyabiashara wao wanaunga mkono, ita—itawabidi kwa namna fulani kujifanya wazuri kwa ajili ya wafanyabiashara.

48 Kwa hiyo sasa tunaona, ya kwamba kule ndani, nilikuwa na mkutano. Usiku huo waliporudi kuja huko kwenye Moteli ya Flamingo, nikasema, "Ninawaonea haya ninyi watu." Nikasema, "Ni fedheha. Kuhusu yote mliyozungumza, mbele ya viongozi wote wa siasa na kadhalika, na wafanyabiashara huku na huko hapa, ilikuwa ni kuhusu, 'Nilikuwa na biashara ndogo sana hapa, na nina kadilaka kumi na sita,' ama chochote kingine zaidi." Nikasema, "Hao watu, hamwezi kujilinganisha nao."

49 Hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi, mnajaribu kujilinganisha na Hollywood. Mnajaribu kulifanya kama Hollywood. Kumbukeni, Hollywood humweka, bali Injili hung'aa. Hamwezi kwenda kwenye ardhi yao; inabidi mwalete mahali tulipo sisi. Hapo ndipo tunapopaswa kuwaleta. Inabidi kuwaleta huku, sio sisi twende kule. Tusingeweza kamwe kujilinganisha nao. Hatutaki kufanya jambo hilo. Wanawaka na kumetameta; Injili inang'aa kwa upole na unyenyekevu. Hiyo ndiyo tofauti kati ya kung'aa na mweko.

50 Sasa tunaona, niliwaambia watu hawa, nilisema, "Jambo lenyewe ni kwamba, ninyi watu ambao ni wafanyabiashara tu, mnajaribu kuhubiri Injili. Si kazi yenu kufanya hivyo. Sisi wahubiri tuna wakati mgumu wa kutosha wa kuiweka sawa. Na ninyi watu hampaswi kuwa mkifanya jambo hilo. Mnajaribu kupachukua mahali pengine. Ninyi ni wafanyabiashara, bali msijaribu kupachukua mahali pa Injili.

51 Ndipo ni—nikasema, "Jambo lenyewe ni kwamba, siku hizi, mnajaribu kusema mna kiasi gani cha utajiri. Ni tofauti jinsi gani na wale wapentekoste wa kwanza! Wapentekoste wa kwanza waliyatoa waliyokuwa nayo."

52 Maskini mwimbaji mmoja pale, alikuwa ni maskini mtu mzuri. Ninampenda. Alikuwa ni mtu mzuri, bali alisema, "Ndugu Branham, kamwe sipendi kukanusha neno lako, wala kusema jambo lo lote dhidi Yake."

53 Nikasema, "Hilo ni sawa. Kama si Neno la Bwana, basi una haki ya kufanya hivyo, ndugu."

Ndipo akasema, "Huo ndio wakati mmoja unakosea."

54 Nikasema, "Loo, la. La, la." Nikasema, "Wapentekoste wa kwanza waliuza kila kitu walichokuwa nacho, na kuviingiza kwenye misheni, na—nao wakatoka wakaenda."

55 Na mhubiri mmoja pale, akasema, "Hilo lilikuwa ndilo jambo baya zaidi walilopata kufanya."

Nikasema, "Ati nini? Ati Roho Mtakatifu afanye kosa?"

56 Akasema, "Sisemi hivyo; bali lilikuwa ndilo jambo baya sana walilopata kufanya." Kasema, "Basi wakati ule mzozo ulipotokea kanisani, hawakuwa na nyumba za kwenda kuishi."

57 Nikasema, "Hiyo ndiyo sababu hasa Mungu aliwafanya wauze nyumba zao, ndipo wakaenda kila mahali, wakiusambaza ujumbe kote nchini. Hawakuwa na mahali pengine pa kwenda." Mungu anajua analofanya, mwacheni tu aendeshe Shughuli Yake.

58 Tunaona kwamba mtu huyu alichukua chetezo, akaingia ku—ku—kuanza ku—ku—kubembeza, che—che—chetezo, kufukiza uvumba. Hiyo haikuwa kazi yake. Yeye alikuwa ni mfalme, si kuwa kuhani. Ndipo kuhani akamkimbilia, na kumwambia, akasema, "Hupaswi kufanya jambo hili. Mlawi ndiye tu anayepaswa kufanya jambo hilo, na wewe si Mlawi. Inatakiwa mtu aliyewekwa wakfu kwa ajili ya jambo hilo, nawe hujawekwa wakfu kwa Bwana. Wewe ni mfalme. Mungu anakubariki. Hilo ni jambo zuri. Bali hujawekwa wakfu kufanya jambo hilo."

59 Mara nyingi sana tumeona watu wakijaribu kuiga karama, wakati hawakuwa wamewekwa wakfu kwa wito huo. Na tumeona mambo yote haya. Tunaona jambo hilo leo kama tu ilivyokuwa wakati huo, kuona mtu fulani akijaribu kumwiga mtu aliye na Roho Mtakatifu; akipiga makelele kama wao, akinena kwa lugha kama wao, na hata hivyo hawajui zaidi juu ya Mungu kuliko Mhotentoti angeweza kujua kuhusu hekaya za Kimisri. Hiyo ni kweli, ni uigaji tu, wakitenda kama kitu chenyewe, wakijifanya kitu fulani.

60 Lakini hebu niwaambie, ninyi mnaoangalia jambo hilo, kumbukeni, pale mnapoona mtu fulani akiiga jambo hilo, kuna kitu fulani halisi mahali fulani. Kama niliokota dola, na ilikuwa ni ya bandia, ni ishara tu ilikuwa imeigizwa kutokana na iliyo halisi.

61 Lakini tunamwona mtu huyu, Uzia, akijaribu kupachukua mahali pa kuhani huyu. Na wakati walipomkimbilia, kumwambia, alikasirika. Aligeuka na kuwaelewesha, "Nitafanya ninalotaka kufanya. Ninyi ni akina nani kuniambia la kufanya? Mnaniambia mimi yale ninayopaswa kufanya? Mimi ni mfalme, nitafanya ninayotaka kufanya!" Ndipo Mungu akampiga kwa ukoma, papo hapo. Ndipo akafa, mwenye ukoma. Katika hasira yake, wakati alipoghadhabika sana, ndipo alipigwa kwa ukoma.

62 Ndipo lilikuwa ni somo kwa nabii huyo kijana, hakika kabisa. Baada ya kumwangalia mtu huyu akifanikiwa, na kupata Ph.D. yake, LL.D. yake, na kadhalika, halafu kujaribu kuchukua mahali pasipokuwa pake. Yeye alikuja kutambua, na akaghadhabikia jambo hilo. Wakati mtu fulani alipojaribu kumwambia kile kilichokuwa ni BWANA ASEMA HIVI, yeye alishindwa kutambua jambo hilo. Ndipo Mungu akampiga kwa ukoma, ambao ni mfano wa dhambi. Vema, kwa jambo hili, Isaya alijifunza kwamba Mungu humpangia mtu Wake kwenye nafasi yake. Mungu ndiye anayepanga. Hatuwezi kumchukua mtu wakati mwingine na kumpangia nafasi.

63 Kijana mmoja mwanamke, hapa si muda mrefu uliopita, aliniambia alininii . . . ama alikuwa na mvulana mdogo aliyekuwa akienda kuninii . . . Alisema, "Mvulana huyo alijisikia alikuwa na wito." Mwanamke huyu alikuwa na umri wa miaka kama thelathini na mitano, nadhani. Akasema, "Mwanangu, mwenye umri wa karibu miaka kumi na minne, yeye anajisikia ana wito. Ndugu Branham, je! ungempeleka aende akapate Ph.D. yake, ama kitu kinginecho kama hicho, kumpeleka kwenye chuo fulani? Ungeshauri nini?"

64 Nikasema, "Kilicho bora sana nijuacho ni chuo cha kwenda magotini, aende magotini." Nikasema, "Angetoka aende miongoni mwa hivyo, na, muda si muda unajua, ataanza kujifunza hesa- . . . hesabu na mambo yote kuhusu *hili*, na hivyo kuhusu *hili*, na wampe mtihani wa akili na wa Kiwango cha Akili, na yote namna hii. Halafu ndipo wamechukua yote ya Mungu, yaliyowahi kuwa nayo ndani yake, wakayatoa," nikasema. Sio kuvidhilisha vitu hivyo hata kidogo, bali ninawaonyesha tu jinsi wanavyoenda mbali sana nje ya mstari.

65 Angalia na uone ni kitu gani, hili lilitukia. Sasa, Mungu humpangia mtu Wake mahali pake.

66 Si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikisoma hadithi ndogo ambapo mwa—mwanamke ambaye alininii . . . aliyekuwa na u—ugonjwa, ni—ni—ni—nimonia, kule Saint Louis, Missouri. Naye alikuwa ni mgonjwa, mgonjwa sana sana, nao wakasema a—a—atakufa. Naye alikuwa na mwanawe aliyekuwa chuoni. Kwa hiyo akaja kutambua, daktari alitambua, ni muda gani zaidi alidhani huyo mama alikuwa nao, wa kuishi. Naye akasema, "Labda hatakuwa hapa kwa zaidi ya siku moja ama mbili, zaidi."

67 Kwa hiyo wakamtumia telegramu kijana mwanamume huyo, kwamba "afadhali uje nyumbani," mama yake alikuwa mahututi kabisa. Kwa hiyo kijana mwanamume huyo, alipoipata hiyo telegramu, alikuwa akijiandaa kwenda, ndipo akapata telegramu nyingine, "Mama yako ana nafuu sasa, ni mzima. Usije."

68 Vema, ndipo yapata mwaka mmoja baadaye, mbona, mvulana huyo akafanya ziara yake ya kila mwaka nyumbani.

Alipokuja nyumbani, akasema, “Mama!” Baada ya yeye kumwamkua, akasema, “Unajua, ninashangaa tu, wakati ulipokuwa mahututi, kamwe hukuniambia kilichotukia.”

69 Akasema, “Loo, mwanangu, nina jambo fulani la kukwambia.” Kasema, “Je! unajua ile misheni ndogo hapa chini mtaani, hapa chini ambapo hao watu wanapiga makelele namna hiyo, na kulia na kuendelea?”

Kasema, “Naam.”

70 Kasema, “Mchungaji wao anaamini katika kuwaombea wagonjwa.” Kasema, “Mmoja wa akina mama hao alikuja hapa na kuniambia.” Akasema, “Daktari aliniambia nilikuwa na siku zingine kadhaa za kuishi.” Kisha akasema, “Ndipo wakatuma habari na wakampata, walitaka kumleta mchungaji huyu aje aniombee, na mama huyo akafanya hivyo, nami nikasema, ‘Vema, hakika, acha aje.’” Kasema, “Unajua, alikuja na,” kasema, “alisoma Andiko kutoka katika Biblia pale.” Kisha kasema, “Alikuja na akaniwekea mikono, na akaniombea. Na, unajua, homa ikaniacha, nami nikapona.” Ndipo mama huyo akasema, “Loo, Mungu asifiwe!”

Akasema, “Mama, mama, sasa unajua vema kuliko hivyo!”

71 Kasema, “Loo, loo, la, la, mpenzi,” kasema, “kweli ilitukia.” Mama huyo akasema, “Utukufu kwa Mungu! Kweli kabisa,” akasema.

72 Akasema, “Sasa kwa kweli uko kama walivyo hao watu.” Kasema, “Haikupasi kufanya hivyo, mama.”

73 Kasema, “Lakini,” kasema, “kipenzi, yeye alisoma hayo moja kwa moja kutoka kwenye Biblia. Alisoma hapo, Marko mlango wa 16, ‘Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.’ Hii hapa, papa *Hapa*.” Kasema, “Sisi, sisi . . . Ndilo hili papa *Hapa*,” akasema.

74 “Loo, mama, hao watu huko ni wale wasio na elimu.” Kasema, “Watu hao kule hawana elimu.” Kasema, “Hao ni watu maskini tu, takataka kama watu wa mitaani, na kadhalika, nao wanakimbilia kule.” Kasema, “Mchungaji huyo . . . ” Kasema, “Tunajifunza huko chuoni, ya kwamba Marko 16, kutoka kwenye kifungu cha 9 na kuendelea, haijavuviwa.”

Mama akasema, “Utukufu kwa Mungu!”

Kijana akasema, “Mama, una nini?”

75 Kasema, “Nilikuwa nikiwazia tu, mwanangu, kama Mungu anaweza kuniponya kwa Neno lisilovuviwa, Yeye angeweza kufanya nini hasa na lile lililovuviwa?” Kwa hiyo ninafikiri hilo kwa namna fulani linamaliza ubishi. Sivyo? “Kama lisilovuviwa litaponya, lile lililovuviwa litafanya nini?” Jambo ndilo hilo, marafiki zangu. Naam, Bwana.

76 Sasa, kujaribu kupachukua mahali pa mwingine. Mungu humweka mtu Wake. Mungu huweka mtu Wake mahali pake. Hapaswi kujaribu kupachukua mahali pa mwingine. Haikupasi kufanya jambo hilo.

77 Sasa lile ono kule hekaluni. Kule hekaluni, alishuka akaenda wakati alipojua hivyo. Isaya aliona jambo hilo, Hezekia, ni kitu gani kilichokuwa kimempata, halafu basi alikuwa amekufa na kulikuwa na ni—ninii . . . Ninamaanisha Uzia, naye alikuwa—alikuwa amepelekwa kwenye kambi ya wenye ukoma, na ilibidi mwanawe atawale mahali pake. Ndipo kwa namna fulani Isaya akachoka, kwa hiyo akashuka kwenda hekaluni siku moja, apate kwa namna fulani kuondoa wasiwasi aliokuwa na—nao.

78 Nafikiri hilo ni jambo zuri kwa sisi sote kufanya, ni kushuka kwenda kwenye nyumba ya Mungu, kushuka kwenda kuiweka huru nafsi yako, kutoa kitu hicho mawazoni mwako.

79 Kwa hiyo Isaya alishuka kwenda kule na akaanza kuomba. Yeye hakuninii . . . Huenda ilikuwa ni kwenye saa za alasiri, naye . . . ama asubuhi na mapema, sijui. Kwa hiyo akapiga magoti madhabahuni na akaanza kuomba, naye akaendelea kuomba mpaka akazama kabisa katika maombi. Sasa hivyo ndivyo inavyopaswa. Alikuwa ameona kile alichokuwa akiangalia, hapa duniani, kimeshindwa. Yule mfalme ambaye Mungu alikuwa amembariki, mfalme huyu mkuu, mwenye nguvu kuliko wote nchini, na hata hivyo alikuwa ameshindwa. Na halafu yeye hakujua la kufanya, ndipo akaingia katika kuomba.

80 Ndipo, mara, akainua kichwa chake, na ndipo akamwona Mfalme halisi. Alimwona Mungu ameinuliwa Juu; pindo za vazi Lake zilizijaza Mbingu. Aliona, aliona kitu cha kuangalia, mfano halisi. Unapoangalia na kujaribu kumfanya mwanadamu kuwa ndiye mfano wako, hakika utakosea, maana yeye atashindwa. Lakini Yeye alikuwa akijaribu kumwambia nabii huyu, "Usimwangalie mwanadamu wala yale asemayo mwanadamu. Geuza macho yako uyaelekeze Kwangu na yale niliyosema. Angalia Hapa juu; si kiti cha enzi cha duniani, bali Kiti cha Enzi cha mbinguni, kilichoinuliwa huko mbali sana Mbinguni," na pindo za vazi Lake zilizijaza mbingu. Ndipo akaangalia juu. Na kisha akaangalia hekaluni, huko hekalu akamwona Mungu ameinuliwa juu, na akawaona Maserafi wa Mbinguni.

81 Sasa, Maserafi pale si Malaika. Wanachukuliwa kuwa ni wateketezaji wa dhabihu wanaomwombea mwenye hatia. Nao walikuwa ni wateketezaji wa dhabihu.

82 Kifuniko maalumu kilikuwa juu ya Viumbe hawa, na kikionyesha ya kwamba Mungu ni mtakatifu kabisa. Mungu ni mtakatifu kabisa. Nao walikuwa wakipaza sauti kwa nguvu zao zote, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni Bwana Mungu

Mwenyezi. Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu," papo hapo mbele za Mungu.

83 Kumbuka, ilikuwa ni Maserafi na Makerubi ambao hulinda Mahali Patakatifu. Hao ndio wanaochukua dhabihu na kuitoa. Nao walikuwa ndio hawa hapa, wakiishi papa hapa Mbele za Mungu, wakiita kwa sauti kuu, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni Bwana Mungu Mwenyezi."

84 Hebu na tuangalie walivyoumbwa kwa muda kidogo. Tunaona ya kwamba hawa walikuwa ni Viumbe wenye mabawa sita. Walikuwa wamefunika nyuso Zao kwa mabawa mawili, mawili juu ya miguu Yao, nao walikuwa wakiruka kwa mabawa mawili.

85 Wazieni, mabawa mawili juu ya nyuso Zao, kwanza. Kwanza, itakuwa ni nini? Hebu na tuone mabawa mawili juu ya nyuso Zao yalimaanisha nini. Mungu akiwa ni mtakatifu sana hata Malaika watakatifu na Makerubi wanapaswa kufunika uso Wao, kusimama Mbele Zake, je! sisi nasi tutasimamaje? Tunaposimama, sote inatubidi kusimama, Mbele za Mungu; Yeye ndiye Hakimu mkuu, nasi sote tutasimama Mbele Zake. Na Malaika watakatifu ambao hawakujua kabisa dhambi ni nini; Wao waliumbwa wakiwa ni Kiumbe maalum, na ili kusimama Mbele Zake, inawabidi kufunika nyuso Zao takatifu, ili kusimama pale. Ikiwa malaika inawalazimu kufunika nyuso Zao takatifu, ili kusimama pale, je! sisi tutafanya nini, kupaswa kuishi Mbele za Mwenyenzi Mungu, kama tukikaa Mbele Zake? Tuna kifuniko, hata hivyo, Damu ya Yesu Kristo. Hiyo ni kweli. Leo . . .

86 Huo ni uchaji. Hilo lilimaanisha uchaji, katika Uwepo wa Mungu.

87 Siku hizi hakuna uchaji. Loo, ule mdogo uliopo, ni mdogo sana. Nini? Unaona watu wakicheka kile kinachoitwa Ukristo. Kitu gani kitampata mtu huyo? Wakati Mungu anapotuma kitu fulani duniani, nao wanakiona kikitenda kazi sawasawa kabisa kwa Neno, na halafu mtu anakinenea isivyo, na kukidhihaki? Unajua vile Biblia ilivyosema? Yesu alisema, "Ni kumkufuru, Roho Mtakatifu, wala hakutasamehewa."

"Loo," wao wanasema, "Hilo ni la ibilisi."

88 Kuwa mwangalifu kwa kile unachosema, ndugu, dada. Kuwa mwangalifu kwa kile unachosema, ewe mwenye dhambi. Hakuna msamaha kwa jambo hilo. Yesu alisema, "Kusema neno dhidi Yake, hakutasamehewa katika ulimwengu huu wala katika ulimwengu ujao."

89 Angalia kile ambacho ndio kwanza amalize kufanya, kutambua, kuwaambia mawazo yaliyokuwa moyoni mwao. Nao walisema, "Yeye ni Beelzebuli," wakimwita Roho wa Mungu "roho mchafu, ibilisi akifanya kazi ya Mungu."

90 Naye akasema, "Nitawasamehe," ule upatanisho haukuwa umefanywa wakati ule, bali, wala Yesu hakuwa amekufa. "Lakini," kasema, "Roho Mtakatifu atakapokuja, kusema neno dhidi ya Huyo, hutasamehewa kamwe." Wakati Roho Mtakatifu atakapokuja kufanya kazi ile ile aliyokuwa akifanya wakati huo, halitasamehewa kabisa. Watu wasio na kicho! Tunaweza kutarajia kitu gani ila hukumu, taifa hili ambalo limemkataa Mungu?

91 Taifa hili, kadiri akina Billy Graham wengi na akina Oral Roberts wengi ambao wamelipua kote humu nchini, na askari wengine wakuu wa Msalaba ambao wamepita katika nchi hii, wakiihubiri Injili, na nchi hii inakengeuka kila mwaka, dhambi inazidi kuongezeka.

92 Ilikuwa ni yu—yule mwinjilisti mkuu, Billy Graham, aliyesema hivi majuzi katika mmoja wa mikutano yake, wakati alipokwenda New York, alisema aliamini "New York ilikuwa imeongezeka asilimia nyingi, katika dhambi, tangu afanye ufufuo wake kule." Kasema wakati alipokuwa hapa California, Los Angeles, alisema, "Katika miaka kumi ama kumi na tano tangu sasa, kwamba kila mwananchi itambidi kubeba bastola, ama kitu fulani cha kujilinda nacho, hawawezi kusimamia sheria vya kutosha, dhambi imepamba moto kwelikweli."

93 Loo, ni kitu gani? Ni kutoiheshimu Biblia. Wameikataa nafasi yao. Wameikufuru na kuidhihaki. Hiyo ni kweli.

94 Sasa hebu na tulitilie mkazo zaidi, angalia makanisa, kile yamefanya. Wengi wao wakienda kote nchini . . . Unapompata mtu akiwa na ninii ya kutosha ya—akiwa ana nguvu halisi za Mungu za kutosha kwake, kuwaambia watu juu ya njia zao za dhambi! Kumpata mtu ambaye atawaambia wanapaswa kuzaliwa mara ya pili, si kupeana mikono wala kuja na kukata kauli. Hawana budi kuzaliwa mara ya pili; si kuandika jina lako kwenye kitabu, wala kujiunga na kanisa, wala kupeana mikono, wala kunyunyizia ko kote, wala ubatizo fulani. Bali ni kuzaliwa na Roho wa Mungu, kutengwa, Uhai wa Mungu ukiishi ndani yako, ukijionyesha wazi; si leo tu, kesho, bali siku zako zote zilizosalia; kwa furaha katika majaribu yako na mateso yako, ungesonga mbele, ukijua ya kwamba barabara imefunguliwa mbele zako, ya kwenda Utukufuni. Ni Injili ya namna hiyo! Unapowapata wa namna hiyo, unaihubiri; ndipo unarudi mwaka ujao, hao hapo wako vile vile, jambo lile lile, ila tu ni wabaya zaidi, na inazidi kuongezeka na kuongezeka. Kadiri unavyohubiri dhidi yake, ndivyo hali inavyozidi kuwa mbaya. Ni kitu gani? Ni ukosefu wa heshima.

95 Na hivyo basi asilimia tisini na tano ya watu hao wanaenda kanisani, wameandika majina yao kwenye kitabu, wanadai kuwa ni Wakristo. Watu wanadai kuwa ni Wakristo, ambao wanavuta sigara, na kunywa pombe, na wanacheza kamari,

na wanafanya mizaha michafu. Mashemasi wengi kwenye halmashauri, wakiwa na mke mmoja, wawili, na watatu, na wanne. Hiyo ni kweli. Ni fedheha jinsi gani! Wanawake wanaimba kwenye kwaya, huku wamekata nywele. Biblia ilisema, "Mwanamke huyo si wa heshima." Rangi usoni mwao! Kulikuwa na mwanamke mmoja tu aliyewahi kujipaka uso rangi, katika Biblia, huyo alikuwa ni Yezebeli. Mungu alimtoa akaliwa na mbwa, kwa hiyo unaona jinsi anavyoliwazia jambo hilo. Halafu unakuja unawaambia kuhusu jambo hilo; mwaka ujao, unarudi, ni wabaya zaidi kuliko walivyokuwa mara ya kwanza. Hawana kicho, hawana heshima, ha—hawana mawazo ya uadilifu.

96 Hebu niwaambieni jambo fulani, enyi wanawake, wasichana, na wazee, pia; mnaotoka hapa nje mmevaa hizi nguo, nguo hizi fupi na chafu zinazobana, na kaptura. Mnasema, "Hupaswi kuwa unazungumza namna hiyo, Ndugu Branham." Napaswa. Huo ni wajibu wangu. Hii ni ninii—hii ni mimbara.

97 Mtu fulani alinipigia simu, si muda mrefu uliopita, mmoja wa wainjilisti wa Kipentekoste walio maarufu sana nchini. Alisema, "Usiwasumbue watu hao."

Nikasema, "Wewe ni nani kuniambia nisiwasumbue?"

98 Akasema, "Ninakupenda." Kisha akasema, "Huduma yako ni ya kuwaombea wagonjwa."

Nikasema, "Ni ya kuhubiri Injili, ndugu."

99 Naye akasema, "Angalia, Ndugu Branham," akasema, "mbona, hao watu wanakuamini kwamba wewe ni nabii."

Nikasema, "Sikusema kamwe kwamba mimi nilikuwa ni nabii, sivyo?"

100 Akasema, "Lakini wao wanaamini kwamba wewe ni nabii. Mbona usiwafundishe hao wanawake jinsi ya kumpokea Roho Mtakatifu, na jinsi ya kupokea vipawa na kufanya jambo fulani, badala ya wewe kuwakemea daima kuhusu jinsi wanavyovaa na yale wanayofanya? Kwa nini usiwafundishe mambo ya namna hiyo, kusaidia jambo hilo."

101 Nikasema, "Ninawezaje kuwafundisha aljebra wakati hata hawatajifunza ABC zao?" Je! mnajua ABC ni nini? Daima mwamini Kristo. Hiyo ni kweli.

102 Sasa, sasa unawezaje kufanya jambo hilo, unawezaje kufanya jambo hilo? Inaonekana kana kwamba wanashinikizwa, kitu fulani hakitawaruhusu kufanya jambo hilo. Inakuwa ni Sodoma ya kisasa. Tuko kwenye saa ya jinsi hiyo., mambo hayo mabaya sana yanayoendelea nchini leo.

Basi akasema, "Vema, angalia . . . "

103 Nikasema, "La, mimi sina miradi ya kufadhili. Sina kanisa la kunifukuza. La, bwana." Nami nikasema . . .

Akasema, “Hiyo ni kazi ya mchungaji, kufanya jambo hilo.”

Nikasema, “Lakini wao hawalifanyi.”

104 Basi, ni wajibu wa mtu fulani, sauti fulani haina budi kupinga jambo hilo, kwa sababu ni baya. Hakika ni baya. Kicho, liheshimuni.

105 Msichana mmoja aliniambia wakati mmoja, alisema, “Bw. Branham, hawashoni nguo zingine ila hizi.”

106 Nikasema, “Wangali wanauza vitambaa, na wana cherehani.” Hiyo ni kweli.

107 Hebu nikwambie jambo fulani, ewe mama. Unaweza ukawa msafi tu na mwadilifu uwezavyo kuwa. Unaweza ukawa mwadilifu vilivyo kwa mumeo, rafiki yako mvulana, uwezavyo kuwa. Lakini moja ya siku hizi, kwenye lile Baraza la Hukumu, itakubidi kuwajibika kwa kufanya uzinzi.

“Iwapo mimi sina hatia?”

108 Una hatia! Yesu alisema, “Mtu yeyote akimwangalia mwanamke, kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake.” Na wakati mwenye dhambi huyo alipokuangalia namna hiyo, na akawa na hayo mawazo kukuhusu wewe, itambidi kuwajibika kwa jambo hilo, kwenye Siku ya Hukumu. Na ni kwa nini alifanya jambo hilo? Ulijianika mbele zake, ukajinengua ukiwa umevaa namna fulani za nguo na mambo kama hayo. Kweli. Ni fedheha. Itakubidi kuwajibika, mama.

109 Na ninyi wanaume mnaojiita Wakristo, ambao mnapaswa kuitawala nyumba yenu, na kuwaacha wanawake wenu wafanye hayo, tubuni, la sivyo nyumba yenu yote itaangamia!

110 Huenda msinipende baada ya jambo hili, lakini nitawaambia Ukweli, maana mikono ya—yangu itakuwa huru na damu hiyo wakati nitakapofika Hukumuni. Hilo ni jambo moja la hakika, unaona. Naam. Sikiliza, ndugu, daima kuna sauti inayoandamana na hiyo ishara, unajua, na ni heri uisikie; si yangu, bali Hivi ndivyo Biblia ilivyosema. Hiyo ni kweli. Loo, ninajua linasikika ni Jambo la mtindo wa kale, bali hivyo ndivyo hasa Biblia ilivyosema, na hivyo ndivyo tunavyopaswa kuwa.

Inabidi malaika kufunika nyuso zao, kusimama Mbele za Mungu.

111 Na, wanawake, wakati Biblia iliposema, “Ni jambo lisilopaswa, ama ni jambo linalopaswa, kwa mwanamke hata kuomba akiwa amekata nywele zake.” Hana haki ya kuomba, nanyi mnamweka kwenye kwaya na hata mnamfanya mhubiri. Hiyo ni kweli.

112 Ninajua jambo hilo linawafanya kuchefukwa moyo kidogo. Lakini, mnajua, kama vile mama alivyozoea kuniambia, kuhusu kunywa kastoroli, “Kama haikuchefui moyo, haikufaidii kitu.” Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo kwa Injili. Inabidi ikufanye uanze

kuwazia. Ni Kweli. Mwanamume na wanawake, wote wawili, wote wana hatia, pande zote mbili, sita upande mmoja na nusu dazani upande huo mwingine.

113 Hapo ndipo mahali tunaposimama hasa, kutokuwa na kicho, haidhuru Neno linasema nini. "Vema, ni sawa. Ninaamini ni sawa." Unabahatisha kwamba ni sawa. Biblia ilisema si sawa! Na *kubahatisha* ni "kujasiria bila amri." Huna amri ya Mungu kulifanya.

114 Seminari hizi na shule na kadhalika, zinazovuka mambo haya namna hiyo, ni fedheha. Inamweka kijana, wahudumu vijana, kwenye njia mbaya, zinawaondoa na kuwapeleka kufuata thiolojia ya kujibunia badala ya Neno la Mungu. Si ajabu hawawezi kuamini Ujumbe halisi wa kweli, si ajabu hawawezi kuwa na mambo Haya kanisani, si ajabu inawabidi kumweka nje katika siku za mwisho, hawana uchaji Mbele Zake. Uwepo Wake unaweza kushuka, watacheka na kulipua chingamu, watembee huku na huko kila mahali na kufanya sijui nini, hawana hata chembe yoyote ya uchaji, Uweponi Mwake. Sasa, sasa hawana uchaji, hata kidogo, kwa Mungu wala kwa watu Wake.

115 Kwa nini, kwa nini wanafanya jambo hili? Sasa sikilizeni kwa makini. Wanafanya hivyo kwa nini?Hawatambui Uwepo Wake. Hawadhani ni Mungu.

116 Je! unafikiri mwanamke huyo kwa kweli angeninii . . . ama yule askari angelimpiga kofi usoni, na angemfunga tambara usoni Mwake na kumpiga kichwani, na kusema, "Sasa kama Wewe ni nabii, twambie ni nani aliyekugusa"? Kama mtu huyo angelijua huyo aliyekuwa akimpiga alikuwa ni Mungu, je! unafikiri angelifanya hilo? Je! unafikiri yule askari mlevi angaling'oa ndevu toka usoni Mwake, na kumtemea mate usoni, pamoja na kuukoholea na kuutemea mate huo uso, kama angalijua huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu? Hakuwa ana habari na jambo hilo.

117 Na leo, kile watu wanachoita kundi la walokole, hawatambui ya kwamba huyo ni Roho Mtakatifu akifanya kazi katika hao watu. Nao wanafanya tu lolote; bila kuuhisi, bila kuuhisi Uwepo Wake. Unajua, kama vile ule msemo wa kale ulivyo . . . Baadhi yao wanasema, "Ninaenda mkutanoni na kucheka, ninaenda mkutanoni kutafuta kosa." Imesemwa ya kwamba wajinga watatembea na viatu vya njumu mahali ambapo Malaika wanaogopa kukanyaga. Hawana ufahamu wa Mungu, hiyo ndiyo sababu.

118 Kwa nini usiwe kama Daudi. Daudi alisema, "Ninamweka mbele zangu daima." Hiyo ndiyo sababu yeye alisema, "Sitaondoshwa," kwa kuwa Mungu yuko daima mbele yake. Naam, bwana.

119 Sasa, pili, walifunika miguu yao. Ilimaanisha nini, "Walifunika miguu yao"? Unyenyekevu. Kufunika nyuso zao kulimaanisha uchaji mbele za Mungu. Kufunika miguu yao kulikuwa ni unyenyekevu Mbele Zake.

120 Kama vile Musa Mbele Zake, akivua viatu vyake, akafunua miguu yake.

121 Paulo wakati alipompata Yesu, ile Nguzo ya Moto, alianguka ardhini, akaanguka chini. Mahali ambapo miguu yake ingelipaswa kuwa, ndipo alipoweka uso wake, unyenyekevu.

122 Yohana Mbatizaji, yule nabii mkuu, wa kwanza kuwa nchini katika muda wa miaka mia nne, bali yeye alisema, "Sistahili kugusa miguu Yake, kufungua gidamu iliyo kwenye viatu vyake."

123 Unaona, kile kilichokuwa juu ya miguu yake, kilichoifunika, kilimaanisha unyenyekevu. Mwangalieni mtumishi huyu sasa mbele za Mungu: uso Wake umefunikwa katika uchaji, miguu Yake imefunikwa katika unyenyekevu, naam, na akitambua sana ninii . . . Utambue sana udogo wako.

124 Sisi sote tunajaribu kuwa mtu fulani mkubwa. "Mimi ni daktari *Fulani*, yule *Fulani* mkuu wa Fulani." Wewe si kitu. Hiyo ni kweli. Hiyo ni ninii tu . . . Wewe si kitu. Ukitaka kujua jinsi ulivyo mkuu, weka kidole chako katika kidimbwi cha maji na ukitoe, ndipo utafute shimo mahali ulipokitumbukiza. Unaona? Hakuna kitu hapo. Na hivyo ndivyo tulivyo. Mungu anaweza kuishi bila ya sisi, bali hatuwezi kuishi bila ya Yeye. Wewe ni nani? Unaona?

125 Kujitambua jinsi wewe ulivyo mdogo. Njia ya kupanda ni kushuka. "Yeye ajinyenyekezaye atakwezwa; yeye ajitukuzaye atashushwa."

126 Si muda mrefu uliopita nilialikwa huko Chicago, na kundi la watakatifu, kuhubiri. Mhudumu fulani mashuhuri Mpentekoste kule mwenye shahada kama nne za chuo, na kadhalika, naye hakutaka njia yangu ya kijinga ya kuzungumza kule mbele ya halmashauri hiyo kuu waliyokuwa wawe nayo, kwa hiyo alimwalika mtu fulani kutoka kwenye shule mashuhuri ya Biblia kule, aje, shule mashuhuri ya Biblia ya Chicago, ahubiri. Basi mtu huyo akasema sasa yale angefanya, "Apande juu pale na kuwadhalilisha watu hao, kwa karibu kila kitu angaliweza kuwazia, kuhusu jinsi walivyokuwa wamekosea kwa kuamini kulikuwa na Roho Mtakatifu na upuuzi huo wote namna hiyo," mbele ya Wapentekoste. Alitoka akaja pale kifua mbele, na u—ukosi uliopinduliwa, kitu kama suti maalumu ya mlo wa jioni, akatupa mihtasari yake yote jukwaani. Alikuwa amepanga mambo kwa ustadi sana mpaka angeweza tu kuelezea Biblia, wala Mungu hakujua chochote juu Yake.

127 Na muda si muda wajua, wewe . . . Aliona mahubiri yake hayakuwaelea watu. Aliendelea kusema kitu kimoja au kingine

namna hiyo, nao waliketi tu na kuangaliana. Hayakuwaelea watu wa aina hiyo, hao Wapentekoste. Kwa hiyo baada ya kitambo kidogo aliona alikuwa ameshindwa, ndipo akaokota vitu vyake akaviweka kwapani, akatoka jukwaani, ameinamisha kichwa chake, amehuzunika. Mzee mmoja mcha-Mungu aliyeketi karibu na ukuta, akasema, "Kama angelipanda juu jinsi alivyoshuka chini, angalishuka chini jinsi alivyopanda." Na hivyo karibu ndivyo jinsi tu ilivyo, pia.

128 Jinyenyekeze, angalia jinsi unavyoweza kuwa mdogo; si yale unayojua, ni yale usiyojua. Hebu jinyenyekeze mbele za Mungu.

Sasa tunaona, ya tatu, Yeye angeweza kuruka kwa mabawa hayo mengine mawili.

129 Sasa angalia, kwanza, Yeye, katika Uwepo wa Mungu, Yeye alikuwa na kicho, huku amefunika uso Wake. Pili, Yeye alikuwa mnyenyekevu mbele za Mungu, akiwa amefunika miguu yake. Na mabawa yake mengine mawili, Yeye angeweza kuruka, yalimwingiza kazini. Loo, jamani!

130 Mungu alikuwa akifanya jambo gani? Alikuwa akimwonyesha huyo nabii jinsi mtumishi Wake aliyeandaliwa anavyopaswa kuwa. Mungu alikuwa akionyesha, "Hawa ndio watumishi Wangu. Hawa ni Wangu. Angalieni jinsi walivyoandaliwa; wenye uchaji, wanyenyekevu, na wako kazini." Hivyo ndivyo watumishi wa Mungu walivyo. Loo, jamani!

131 Hivyo ndivyo inavyotupasa kuwa: kuwa na uchaji kwa Neno la Mungu, wanyenyekevu, na kazini kwa Mungu.

132 Kama vile yule mwanamke wakati alipoitwa aingie kazini, akaja, wakati aliposema, "Njoni, muone Mtu ambaye ameniambia yale nimefanya."

133 Ishara Yake ilimshawishi, ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi. Akasema, "Bwana, tunajua, Masihi ajapo. . . Sasa, Wewe huna budi kuwa u nabii. Tunajua, Masihi ajapo, Yeye atatwambia mambo haya."

134 Unaona, alimtarajia Yeye aseme, "Vema, Masihi yuaja hivi karibuni sana; mimi ninamtangulia tu." Lakini Yeye alisema, "Mimi Ndiye."

135 Hilo lilimfanya aingie kazini sasa hivi. Aliingia kazini. Usingeweza kumzuia. Ilikuwa ni kama nyumba iliyokuwa inaungua, kama nilivyosema hivi majuzi usiku, katika upepo mkali. Usingeweza kumzuia. Huyoo akashuka kwenda mjini, "Njoni, muone Mtu ambaye aliniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?" Unaona? Alikuwa kazini.

Alifanya nini? Alikuja, kwanza, akajinyenyekeza.

"Nipe maji ninywe."

136 Kasema, “Mbona, baba zetu walikunywa maji kutoka kwenye kisima hiki,” na kadhalika. Na—naye . . .

137 Kasema, “Vema, nitakupa Maji unywe; usije hapa.”

Yule mwanamke, “Bwana, Bwana, nipe Maji hayo.”

138 Unaona, alikuwa mnyenyekevu kuhusu hilo. Na alipojinyenyekeza, ndipo Yesu alipomwonyesha ishara ya Masihi, na hilo likamwingiza kazini. Ndipo akawa tayari kwenda basi, alikuwa tayari kumwambia kila mtu aliyekutana naye. Unaona?

139 Kwa kweli, kuhusu mila za nchi hiyo ya Mashariki, wanaume hao kamwe wasingelimsikiliza huyo mwanamke. Mwanamke kama huyo hana sauti yoyote miongoni mwa watu. Kwa hakika hana. Hawezi kusema kitu. Lakini ati ujaribu kumnyamazisha? Alikuwa kazini. Ilimbidi amwambie mtu fulani, “Njoo huku ukajionee mwenyewe. Mtu huyo aliniambia yale niliyofanya. Je! hilo silo ambalo tumekuwa tukilitarajia? Je! hilo silo ambalo Maandiko yanasema, ya kwamba Masihi, atakapokuja, atafanya jambo hili?” Alikuwa kazini kwa maana alijinyenyekeza, Na Mungu akaingia ndani yake.

140 Petro, alipolichukua Neno Lake. Wakati alipovua usiku kucha, akiwa mvuvi sehemu fulani huko, naye akaingia, amevunjika moyo, hakuna samaki. Mvuvi mzuri yeyote anajua hilo linamaanisha nini, bila samaki. Halafu, jambo la kwanza, alikuwa amesafisha nyavu zake, akawa amezianika ukingoni, na alikuwa akiziacha zikauke.

141 Ndipo Yesu akafika na akaomba kutumia chombo chake. Akahubiri. Kisha akasema; “Simoni, tweka mpaka kilindini, na mkashushe nyavu mvue samaki. Rudini moja kwa moja mahali ambapo mmevua kwa juya, usiku kucha. Rudini moja kwa moja mahali mlipofanya kazi ya kuchosha, saa baada ya saa, na mkashushe nyavu zenu kwa ajili ya mvuo mkubwa wa samaki, mkawavue wengi.”

142 Sasa angalia. Yeye akasema, “Bwana, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu. Lakini kwa Neno Lako, Bwana, nitazishusha nyavu. Kwa Neno Lako!” Hivyo ndivyo inavyotakiwa, amini Neno Lake Mungu. Na wakati aliposhusha ule wavu, alipata samaki wengi mno mpaka wavu huo ukaanza kukatika.

143 Hilo lilimwingiza kazini. Naam, bwana. Ushawishi wa Yesu juu yake ulimwingiza kazini, ndipo akashusha wavu. Ndipo Yesu akasema, “Usiogope, tangu sasa utavua watu.”

144 Yule mwanamume kipofu, wakati alipoponywa, akiketi langoni na . . . ama akiketi mtaani. Nao Mafarisayo walisema, “Mtu yeyote atakayemkiri, ama aliyekuwa na uhusiano wowote na Yesu, atafukuzwa hekaluni.”

145 Wao, wao walikuja, wakamwuliza baba yake na mama. Wakasema, "Yeye ni mtu mzima; mwulizeni."

Akasema, "Mtu, anayeitwa Yesu, aliniponya."

146 Wakasema, "Mtu huyu ni mwenye dhambi. Yeye si wa makundi yetu. Hatujui Yeye ametoka wapi. Mpe Mungu sifa!"

147 Akasema, "Sasa, kama yeye ni mwenye dhambi ama si mwenye dhambi, mimi sijui." Akasema, "Bali najua hili jambo moja; ambapo nilikuwa kipofu, sasa ninaweza kuona." Naye akasema, "Jambo la kuchekesha ni kwamba, kwangu mimi, ya kwamba ninyi mnapaswa kuwa ndio viongozi wa kiroho wa wakati huu, na Mtu huyu aliyafungua macho yangu, na hata hivyo hamjui anakotoka." Yeye alifanya nini? Aliingia kazini. Hiyo ni kweli. Ilimweka kazini, kwa sababu alieneza sifa zake nchini kote.

148 Wale watu, kwenye ile Siku ya Pentekoste, wakati Yesu alipowaambia wangojee kule juu, nao wangeninii... Kushuka, na Roho Mtakatifu aliposhuka juu yao kwenye Siku ya Pentekoste, wakati waliposhawishiwa na Neno la Mungu lililodhihirishwa. Sasa kumbukeni, Yesu alisema, "Ngojeni Yerusalemu mpaka mtakapopata Nguvu zitokazo Juu." Wakangojea, si siku nane, si siku tisa; walingojea kwa siku kumi, mpaka ahadi hiyo ilipodhihirishwa. Ndipo Roho Mtakatifu akashuka na kujigawanya, na ndimi za Moto zikawakalia kila mmoja wao.

149 Na wakati walipokuwa wakishawishiwa na Roho Mtakatifu, waliingia kazini, wakipepesuka kama walevi, wakipiga makelele, wakinena kwa lugha, haoo wakaingia mtaani.

Watu wakasema, "Watu hawa wamelewa chakari kwa mvinyo mpya."

150 Yeye, Petro, akasimama, na akasema, "Jambo hili ni lile lililonenwa na nabii, Yoeli, 'Na itakuwa katika siku za mwisho.'" Ilifanya nini? Ilimwingiza kazini.

151 Itakuingiza kazini, kama hujampata, itakuingiza kazini wakati utakapoona Neno la Mungu likitimizwa. Kile tumeona katika siku hizi za mwisho, kinapaswa kutuingiza kazini. Inapaswa kufanya jambo hilo, kama tungeweza tu kulifanya kwa uchaji na unyenyekevu. Ile Nguzo ya Moto mbele ya Paulo, ilimwingiza kazini. Na leo wakati tunapoona Nguzo ile ile ya Moto, kwa sayansi, kwa kazi Zake, kwa yale iliyoahidi, ikilifanya Neno katika siku hizi za mwisho kutimia sawasawa kabisa, inapaswa kutuingiza kazini. Kwamba, ishara imetolewa, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, kabla tu Sodoma haijachomwa moto, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu; Yeye atadhihirishwa tena, yeye yule jana, leo, na hata milele." Inapaswa kumwingiza kila mshiriki wa Mwili wa Kristo kazini, kuingiza ndani kila kitu unachoweza, maana hii ndiyo saa ya mwisho, ndio wito wa mwisho, wito wa mwisho.

Neno kwa neno, limekwisha kutimizwa. Bila shaka linapaswa kutuingiza kazini.

152 Sisi, kama vile nabii, tumeona matokeo ya madhehebu yaliyojiinua yakipoteza mahali pao katika Kristo, wakishindwa kulishikilia Neno Lake, wakikubali kanuni za imani. Na tuliona kile kilichowapata walipofanya jambo hilo, walikufa kiroho. Tunaona kilichowapata Walutheri wakati walipoukataa wito wa Wesley. Tunaona kile kilichowapata Wamethodisti wakati walipokataa wito wa Kipentekoste. Sasa vipi kuhusu Wapentekoste? Unaona?

153 Tumeona watu waliojitukuza, kama jambo lile lile la Uzia, aliyejaribu kupachukua mahali pa huduma iliyotiwa mafuta. Huduma ya mtu kanisani imetiwa mafuta, si kuchaguliwa. Imetiwa mafuta. Kanisa, m-. . .mchungaji, mwinjilisti, nabii, mtume, haina budi kuwa huduma ya Mungu iliyotiwa mafuta, si iliyochaguliwa na mwanadamu. Mwanadamu alijaribu kuchagua huduma hiyo wakati mmoja, waliipigia kura; maskini Mathiya kamwe hakufanya kitu, bali Mungu alimchagua Paulo naye alifanya kitu kwa sababu alikuwa ametiwa mafuta. Nasi tumeona wahudumu hawa wakijaribu kusema, "*Huyu* ni askofu mtakatifu *fulani*, *huyu* ni mzee *fulani*, *huyu* ni mtu *fulani*," hilo halifiki kamwe popote. Lakini wakati Mungu anapoingia na kuchukua mamlaka, ndipo tunaona upako wa Roho Mtakatifu ukilithibitisha Neno la Mungu.

154 Sasa, matokeo ya hilo ono kwa nabii, je! lilifanya nini kwa mtu huyu aliyezaliwa nabii? Kumbukeni, yeye aliandika Biblia nzima. Kuna vitabu sitini na sita vya Isaya, na vitabu sitini na sita vya Biblia. Inaanza, kama vile katika Mwanzo; katikati ya Kitabu linakuja Agano Jipya, Yohana Mbatizaji; na kuishia katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Nabii mkuu, mmoja wa manabii wakuu sana tuliopata kuwa nao, alikuwa ni Isaya, naye alizaliwa kuwa hivyo.

155 Lakini wakati aliposimama Mbele za Mungu, hilo lilimfanya nabii afanye nini? Nabii alisema, "Ole wangu, kwa maana mimi ni mtu mwenye midomo michafu." Kuja Mbele za Mungu, na kuona chombo cha Mungu cha kweli kilichotiwa mafuta, kulimfanya nabii kukiri ya kwamba yeye alikuwa ni mwenye dhambi. Kunapaswa kutufanya hivyo, kunapaswa, Uwepo wa Mungu wenye mafuta. Wakati alipomwona Huyo akilia, na vile vizingiti vikitikisika, na Malaika hawa wakienda huku na huko, wakithibitisha walikuwa mbele za Mungu, Nao walikuwa ni watumishi wa Mungu, waliotiwa mafuta, Nao wakasema kwa sauti kuu; yeye alikuwa mwenye dhambi.

156 Ilikuwaje basi wakati alipokuwa tayari? Sasa sikilizeni, katika kufunga. Yeye alikuwa tayari kukiri ya kwamba alikuwa ni mwenye dhambi, "Ole wangu, kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wenye

midomo michafu. Ole wangu!" Ndipo Malaika akachukua koleo na kutwaa kaa la moto kutoka madhabahuni, akalishika mikononi mwake, kisha akaja na kumtakasa nalo. Ndipo ukaja utakaso, baada ya kukiri kwake.

157 Sasa kama nabii, aliyeitwa, aliyethibitishwa kuwa nabii wa Mungu, katika Uwepo wa Mungu, akiona udogo wake, alikuwa tayari kukiri ya kwamba yeye alikuwa ni mwenye dhambi, wewe na mimi tunapaswa kufanya nini? Lakini unajua tunachofanya? Tunageuza kichwa chetu, na kuondoka na kucheka. Hapo ndipo tunaposimama, mpaka utakaso utakapokuja. Angalia, Isaya . . .

158 Ninataka mwone kitu kingine. Mungu hakutumia vitabu na thiolojia, maneno ya kithiolojia, kumtakasa mtumishi Wake. Alitumia Moto. Kamwe Yeye hakutumia kanuni za imani kumtakasa mtumishi Wake. Alichukua moto kutoka madhabahuni. Na kama Mungu akimtakasa mtu leo, haina budi kuwa ni Moto wa Roho Mtakatifu unaomtakasa mwanadamu; si kusoma kitabu na kufanya jambo *hili*, ama kitabu fulani kingine cha mtu *fulani*.

159 Mhudumu mmoja fulani mkuu hapa California alisema, hivi majuzi, alikuwa na "kitabu cha mwaka." Sikubaliani naye. Kitabu cha mwaka ni Biblia, kimekuwa ndicho daima. Kitabu cha mwaka ni Kitabu cha Mungu, daima.

160 Basi Mungu alitumia Moto kumtakasa mtumishi Wake. Ndipo ikafuata, baada ya yeye kukiri kwa unyenyekevu ya kwamba alikuwa amekosa, na halafu ukaja utakaso; na baada ya utakaso, ndipo kukaja kule kuagizwa. Unaona, shida ndiyo hiyo, baadhi yetu tunajaribu kupata agizo kabla hatujatakaswa. Unaona? Tutasema, "Vema, nitafuata *hili*." Inatupasa kumfuata Mungu. Hao Malaika walifanya jambo moja, waliishi katika Uwepo wa Mungu; wanyenyekevu, wenye kicho, na kuwa kazini mbele za Mungu. Ndipo linafuata, lile agizo; baada ya kutubu na kutakaswa, hapo ndipo basi ambapo Isaya aliyetakaswa akasema kwa sauti kuu, "Mimi hapa; nitume mimi."

161 Loo, ndugu, dada, kama kulipata kuwa na wakati ambapo akina Isaya wanapaswa kushuka kwenda kwenye nyumba ya Mungu kwa ajili ya kutakaswa! Kama kuliwahi kuwa na wakati ambapo mfuasi wa kanisa anapaswa kwa kweli kuja na kutubu dhambi zake! Kama kulipata kuwa na wakati kwa ajili ya mtu aliyerudi nyuma!

162 Hebu wazia tu, katika ule usiku ambapo Sodoma uliteketezwa, sijui ni watu wangapi waliupa kisogo ujumbe wa wale Malaika? Sijui ni watu wangapi hawakujihusu vya kutosha kuisikiliza sauti Yao? Nao waliangamia usiku uo huo, nao hawatakuwako tena, ila tu hukumu yao katika jehanamu.

163 "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu." Ni watu wangapi waliomcheka na kumdhihaki, na kuja pale kusikiliza tu uninii wake, kasema, "Tutapanda twende tukamsikilize yule mzee

mwenda wazimu akipayuka tena, tupate tu ya burdani kidogo." Wanasimama, wanaondoka, hata wasingemsikiliza akihubiri. Mambo ya kila namna; nao waliangamia katika hukumu alizokuwa akihubiri.

164 Amosi, yule mhubiri mdogo, akijua…kutoka mahali pasipojulikana, nabii, aliyetiwa mafuta, alipanda akaja akaangalia huko chini Samaria wakati ule. Kichwa chake chenye kipara kiling'aa, maskini ndevu zake zenye mvi, alipopanda kushuka kilima. Aliangalia huko chini, hayo macho yake matakatifu yalifinyaa alipoutazama huo mji, si kama watalii wanaotoka ulimwenguni kote. Maana, hao makuhani, wote hao, walikuwa wamefanya dhambi, na manabii wa uongo walikuwa wakiwaambia mambo yako sawa. Alishuka akaenda kule bila ya kuungwa mkono katika ufufuo wake. Alishuka akaenda kule bila kitu chochote, na akapaza sauti kwa nguvu. Na akasema, "Mungu yuyo huyo, ambaye mnadai kumtumikia, atawaangamiza."

165 Nami ninasema BWANA ASEMA HIVI: yule Mungu, ambaye Marekani inadai kumtumikia, ataiangamiza. Chukueni hilo kwa namna yoyote mpendavyo. Tunachohitaji, ni kushuka kwenda pale chini madhabahuni, ewe Isaya. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Ndipo Mungu akasema, "Ni nani atakayekwenda kwa ajili Yangu?"

166 Isaya akasema, "Mimi hapa; nitume mimi." Ninawazia kuhusu wimbo ule:

> Kaa la Moto lilipokuwa limemgusa yule nabii,
> Likimfanya msafi kama usafi ungeweza kuwa,
> Wakati sauti ya Mungu iliposema, "Ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu?"
> Ndipo akajibu, "Bwana, mimi hapa, nitume mimi."

167 Kwanza ilibidi kujinyenyekeza na kutakaswa, na kuwa tayari kama tulivyomwona mtumishi aliyeandaliwa. Mwangalie Uzia jinsi alivyoandaliwa, bali alishindwa. Usiweke…

168 Unasema, "Vema, sasa, ninamjua Daktari *Fulani* ni mtu mzuri. Ninamjua Ndugu *Fulani*." Huenda wakawa, bali usiangalie jambo hilo.

169 Angalia *hapa*, unaona, Njia ndiyo *hii*. Mungu ana njia ya kuandaa. Yeye alifanyaje jambo hilo? Kwenye Siku ya Pentekoste, Petro aliwaambia la kufanya. Aliwaandikia maagizo, na daima yamebaki kuwa vivyo hivyo. Usiyachezeechezee, utamwua mgonjwa wako.

Wakasema, "Tufanyeje tupate kuokolewa?"

170 Akasema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi

mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie."

171 Hilo liko papa hapa usiku wa leo. Kama Mungu angali anaita, hayo ndiyo maagizo. Bado unaweza kumpokea Roho Mtakatifu yeye yule ambaye wao walimpokea pale, ninii tu... Unaweza kupokea kitu kile kile usiku wa leo. Fuatilia tu mpaka mwisho. Hivyo tu ndivyo unavyofanya. Naam, ndipo unaweza kusema:

> Kaa la Moto lilipomgusa yule nabii,
> Likimfanya kuwa msafi kama usafi uwezavyo kuwa,
> Wakati sauti ya Mungu iliposema, "Ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu?"
> Ndipo alijibu, "Bwana, mimi hapa, nitume mimi."

Hebu na tuuimbe

> Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
> Nena, nami nitakujibu haraka;
> Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
> Nena, nami nitakujibu, "Bwana, nitume mimi."

172 Hebu sikiliza hapa, ndugu.

> Kuna mamilioni sasa wako katika dhambi na aibu, wanakufa;
> Loo, sikilizeni kilio chao cha huzuni na uchungu;
> Hima, ndugu, hima ukawaokoe;
> Sasa jibu haraka, "Bwana, mimi hapa."

> Loo, nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
> Nena, nami nitakujibu haraka;
> Loo, nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
> Nena, nami nitakujibu, "Bwana, nitume mimi."

173 Na tuinamishe vichwa vyetu. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nena, Bwana Wangu*—Mh.]

> Likimfanya msafi kama usafi uwezavyo kuwa,
> Hapo sauti ya Mungu iliposema, "Ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu?"
> Ndipo akajibu, "Bwana, mimi hapa, nitume mimi."

Je! unataka kuwa mnyenyekevu na kutakaswa?

Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
Nena, nami nitakujibu haraka;
Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
Nena, nami nitakujibu, "Bwana, nitume mimi."

174 Wakati wanapiga, sasa, je! kuna Isaya mmoja hapa ndani usiku wa leo, ama mia moja, wanaotaka kwenda, wanaotaka utakaso wa Mungu maishani mwako? Ninyi msiomjua Kristo kama Mwokozi wenu, mnaalikwa sasa madhabahuni, kama Yeye ananena na moyo wako. Mimi sipendi sana jambo la kushawishi. Nafikiri Roho Mtakatifu Mwenyewe ndiye anayeshawishi. Bali kama wewe upo hapa, nawe huna Kristo. . . Sasa kumbuka, utawajibika kwenye ile Siku ya Hukumu, kwa yale unayofanya na jambo hili usiku wa leo. Unaona? Sasa kama unataka kuja, mimi niko hapa kuomba pamoja nawe.

175 Katika Jina la Kristo, ninawapa nafasi ya kuja, kumtafuta Mungu, na kwa furaha huenda mkampata. Enyi vijana, wazee, watu wa makamu, wafuasi wa kanisa, yeyote uliye; kama Moto wa Mungu, kwa Roho Mtakatifu, haujakutakasa moyoni mwako, kufikia mahali ambapo unaamini kila Neno la Biblia hii, na Kristo ni shahidi aliye hai wa ninii yako. . . moyoni mwako, kwamba amefufuka kutoka kwa wafu, basi ninakualika madhabahuni. Njoo hapa na hebu tuombe pamoja nanyi. Tukiamini ninyi nyote, basi, kwa matendo yenu wenyewe, ya kwamba mmeokoka.

176 Halafu, je! yupo mtu aliyerudi nyuma hapa ndani ambaye angetaka kuja? Ninawauliza, kama mtumishi wa Kristo, kama mtashuka kuja hapa chini na tuombe pamoja nanyi. Sisemi atawakubali; ninaamini atawakubali. Si mje mkamjaribu hilo sasa? Kama ananena nawe, njoo.

177 Wale wasio na ubatizo wa Roho Mtakatifu? Ninadhani hakuna mmoja hapa asiye nao, ambaye hajarudi nyuma. Kila mmoja, basi, hapana budi ameomba kwa bidii sana; ni Wakristo, na mmeomba kwa bidii sana. Na basi kama umeomba kwa bidii sana, wala huna ule ubatizo, na ungetaka Mungu akupe hilo, ni nafasi yako basi, sasa.

178 Yupo mtu mmoja hapa ambaye hana. Nautakia heri moyo wake mnyenyekevu. Ninatumaini ni Isaya mwingine.

Sasa inueni vichwa vyenu basi.

179 Kuna mtu mmoja aliyeinama hapa madhabahuni, mmoja ninayeamini kwamba ni Isaya.

Sasa Yeye yupo hapa. Je! unaamini Yeye yupo hapa?

180 Sasa nitawaambia yale mliyofanya. Mmefanya jambo baya sana mlilopata kufanya. Kuna watu mia mbili ama mia tatu hapa wanaopaswa kuwa madhabahuni.

181 Hebu niwaonyeshe, katika Jina la Bwana, ya kwamba ninayosema ni kweli. Angalieni. Baadhi yenu ninyi watu hapa, ombeni.

182 Hapa, hapa ameketi bibi aliyevaa koti jeupe, jaketi dogo jeupe, akiniangalia moja kwa moja. Siwezi . . . Yeye ni Mkristo. Bali anaomba kwa ajili ya ugonjwa fulani. Ana yabisi kavu. Je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukupa afya, kukuponya? Basi unaweza kupona.

183 Mtu anayefuata, anayeketi karibu na wewe pale, ana kasoro masikioni mwake. Je! unaamini Mungu anaweza kuponya shida yako ya sikio, bwana, na kukupa afya? Naam. Inua mkono wako kama unaamini.

Sasa tafadhalini iweni na uchaji, kwa kitambo kidogo tu.

184 Mtu aliye papo hapo karibu naye anaumwa ugonjwa wa moyo. Je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukuponya, bwana, wewe uliye na ugonjwa wa moyo? Sikujui. Sikufahamu. Hiyo ni kweli? Wewe ni mgeni. Vema, sikiliza. Kama Mungu angeniambia kwamba wewe ni nani, je! ingekusaidia? Je! mwaweza kunisikia vizuri? Jina lako ni Bw. Blackwood. Je! unaamini Yeye anaweza kuniambia mahali unakotoka? Unatoka Riverbank, California. Kama hiyo ni kweli, simama kwa miguu yako. Sijapata kumwona, maishani mwangu. Vema.

185 Mungu akubariki, bwana. Imani yako ilikuponya. Bibi huyo anayeketi karibu na wewe pale, yeye ana ugonjwa wa wasiwasi. Je! unataka kuponywa wasiwasi wako? Inua mkono wako juu, kama unataka kuponywa. Weka mkono wako juu yake, bwana, apate kuponywa.

186 Bibi anayeketi karibu na wewe, sasa, ana kisukari, aliyevaa gauni jekundu. Anataka kuombewa, pia. Unaona? Anataka kuombewa. Uwe na imani.

187 Huyu hapa mama anayeketi hapa nyuma kabisa. Yeye yuko tayari kufanyiwa upasuaji. Kama tu anaweza kuninii . . . Ee Mungu! Yeye ana kizazi kilicholegea. Jina lake ni Bi Maxwell. Amini. Simama, kubali uponyaji wako, Bibi. Huna kadi ya maombi, sivyo? Huna kadi ya maombi? Vema, huhitaji moja. Inua mkono wako kama hayo ni kweli. Sikujui. Kama hayo ni kweli, punga mkono wako. Sisi hatufahamiani, punga mkono wako namna hii.

Je! yeye aligusa nini? Hakunigusa mimi.

188 Bw. Stewart, je! ungetaka kuponywa, pia, wasiwasi, pia uamini ya kwamba Mungu atakuponya? Hatufahamiani. Lakini hilo ndilo jina lako, nawe unaugua ugonjwa wa wasiwasi. Ni vigumu kwako kujishikilia. Simama kwa miguu yako na ukubali uponyaji wako, katika Jina la Yesu Kristo.

189 Huyu hapa mama mmoja anayeketi hapo nyuma yako pale. Yeye ana wasiwasi, pia. Ana kasoro fulani kwenye misuli mwilini

mwake. Ataukosa na. . .Bibi Newell, simama, kama hilo ndilo jina lako na ndivyo unavyoitwa. Amini! [Dada huyo analia kwa sauti kuu—Mh.]

Je! mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

190 Hakika, huyu hapa mama mmoja anayeketi papa hapa karibu, ana ugonjwa wa moyo na shinikizo la juu la damu. Je! unaamini jambo hilo, ni kweli, dada? Simama kama hiyo ni kweli.

191 Mama anayeketi karibu yako hapo, ana kitu fulani kifuani mwake. Kama hiyo ni kweli, simama.

192 Mwambie huyo mama, aliye karibu naye, ana vivimbe usoni mwake, vitu kama vivimbe. Kama anataka hivyo viponywe, mwambie asimame na kuukubali.

193 Sasa kuna kundi lenu hapa ndani linalopaswa kuwa kwenye madhabahu hii, likimtafuta Roho Mtakatifu. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Mnaona ninalomaanisha? Mara nyingine tena nitatoa wito huu. Hilo ni thibitisho ya kwamba ninasema kweli. Mungu ananena na watu hapa ndani, nanyi kidogo mnalitilia shaka. Je! utakuwa waaminifu vya kutosha kuinua mkono wako, useme, "Naam, Ndugu Branham, daima nimekuwa kidogo siko thabiti. Ninataka sehemu zaidi ya Mungu. Ninajua kuna kitu fulani nisicho nacho hapa ndani, na napaswa kuwa nacho wakati nilipokiri ubatizo wa Roho Mtakatifu"? Inua mkono wako, je! utafanya hivyo? Kuwa tu mwaminifu kwa nafsi yako. Roho Mtakatifu kamwe hakosei. Mbona usije huku, basi, na kutatua shaka hiyo? Njoo! "Nitaninii upesi. . . "

Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu, (naam)
Nena, nami nitakujibu haraka.

194 Unaona, siwaambii jambo la makosa, wapendwa. Ni Roho Mtakatifu akiita. Wako mamia ndani hapa, kama mliamini mimi kuwa nabii. Sasa, kumbukeni, ninawaambia katika Jina la Bwana, mmedanganywa. Njoni!

Kaa la Moto lilipomgusa yule nabii,
Likimfanya msafi kama usafi unavyoweza kuwa,
Hapo sauti ya Mungu iliposema, "Ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu?"
Ndipo alijibu, "Bwana, hapa, nitume mimi."

195 Je! hutasema jambo lile lile? Basi amkeni, inueni mikono yenu.

Nena, Bwana wangu, loo, nena, Bwana wangu,
Nena, nami nitakujibu haraka;
Nena, Bwana wangu.

196 Yeye anafanya nini? Mjibu basi, kama Yeye anazungumza. Kama kuna tashwishi ndogo mahali fulani, wewe huna sasa hakika ya jambo hili, usibahatishe. "Bwana, nitume."

> Loo, nena Bwana wangu, (Yeye ananena. Njoni.) . . . Bwana wangu,
> Nena, nami nitakujibu . . .

197 Sasa, enyi watu, mimi si mwepesi wa ushupavu wa dini. Si mwepesi wa kusema mambo ya uongo. Ninajisikia kuongozwa wakati ninaposema ninalofanya.

> . . . Bwana wangu,
> Nena, nami nitakujibu . . .

198 Unasema, "Watu watasema nini juu ya jambo hilo?" Ni yale Mungu atakayosema juu ya jambo hilo, ndiyo hayo. "Nitume mimi."

> Nena, Bwana wangu, (hiyo ni kweli)
> Nena, nami nitakujibu haraka;
> . . . Bwana wangu, loo, nena Bwana wangu,
> Nena, nami nitajibu, "Bwana, nitume mimi."
>
> Kuna mamilioni sasa katika dhambi na aibu wanaokufa;
> Loo, sikilizeni kilio chao cha huzuni na cha uchungu;
> Hima, ndugu, hima ukawaokoe;
> Loo, jibu upesi, "Bwana, hapa, nitume mimi."
> Loo, nena, . . . wangu,

199 Sasa kila mtu hapa ndani, tunataka kujitayarisha kwa ajili ya ibada kubwa ya uponyaji kesho, pia. Nami ninawataka kila mmoja wenu wahudumu mje karibu na watu hawa wanamtafuta Roho Mtakatifu, msikome tu katika dakika tano, bakini hapo mpaka, (kwa muda gani?) mpaka Roho Mtakatifu atakapokuja.

> . . . Bwana wangu,
> Loo, nena, nami ni- . . .

200 Sasa hebu wasikilizaji sasa weka mkono wako juu ya mtu mwingine, wekeaneni tu mikono ninyi kwa ninyi, juu ya mtu fulani; ninyi ambao mtaomba, mnaowawakilisha watu hawa hapa.

> . . . Bwana wangu,

201 Sasa marefu ya kanisa yamejaa kweli kweli, madhabahu imejaa kabisa, kuna watu wapatao mia moja na hamsini, watu mia mbili.

> . . . Bwana wangu,
> Nena, nami nitaji- . . .

202 Sasa anzeni kuomba, "Bwana, nitume mimi! Nena, Bwana wangu! Bwana, nitume mimi!"

203 Waponye hawa, Bwana, katika Jina la Yesu Kristo. Bwana, tujalie. Ee Mungu, tujalie maombi ya hawa.

204 Usiachilie. Kaa papo hapo mpaka litakapotukia. Kaa mpaka utakaposikia wito wa Mungu. Simama mpaka makerubi wawe wanakutikisa, Roho Mtakatifu ametwaa kaa la Moto kutoka madhabahuni mwa Mungu, analiweka mdomoni mwako.

205 [Ndugu Branham anamwita Ndugu Roy Borders mimbarani—Mh.]

“Nena, Bwana wangu.”

*VISHAWISHI* SWA64-0215
(Influences)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi jioni, tarehe 15 Februari, 1964, katika Ukumbi wa Elliott huko Tulare, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2010 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org